

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

Simu Na: +255 (026) 2963630  
Nukushi: +255 (026) 2963629  
Barua Pepe: [ps@utumishi.go.tz](mailto:ps@utumishi.go.tz)  
Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Menejimenti ya Utumishi wa Umma  
na Utawala Bora,  
Jengo la Taaluma Na. 1,  
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,  
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),  
18 Barabara ya Mkalama,  
S.L.P. 670,  
**40404 DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**TAHADHARI KUHUSU UTAPELI**

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inatoa tahadhari kwa watumishi wa umma nchini, kujiepusha na utapeli unaofanywa na watu wanaojitambulisha kuwa ni Maofisa wa Ofisi Ya Rais-Utumishi kwa lengo la kutaka kuwapa msaada wa masuala mbalimbali ya kiutumishi ikiwemo kuwarejesha katika utumishi wa umma, watumishi waliobainika kuwa na vyeti vya kughushi pamoja na kuwapandisha madaraja.

Matapeli hao hutoa anuani za barua pepe ya [psut@utumishi.go.tz](mailto:psut@utumishi.go.tz), [rwizautmsh@gmail.com](mailto:rwizautmsh@gmail.com) na nukushi; 0262963629 pamoja na namba za simu za kiganjani. Miongoni mwa namba hizo ni 0743911649, 0784365957, 0763736619 na 071534736.

Serikali inawatahadharisha watumishi wa umma na wadau wote kuwa makini na matapeli hao kwani stahili zozote za mtumishi wa umma ni lazima zizingatie Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo katika Utumishi wa Umma.

IMETOLEWA NA:  
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**  
**OFISI YA RAIS (UTUMISHI)**  
TAREHE 31 JULAI, 2018